

HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA
KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI
KILICHOFANYIKA TAREHE 19/11/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA
HALMASHAURI – BUKULU
AGENDA NA. 05

A. WAKUU WA IDARA

- | | |
|---------------------------|--|
| 1. Mustapha S. Yusuph | Mkurugenzi Mtendaji(W) |
| 2. Fred J. Bajale | Kny; Katibu Tawala (W) |
| 3. Eliamini Slao | Kny; Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 4. Mashauri M. Vicent | Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 5. Dr. Christian Mwigwa | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 6. Joshua S. Mnyang'ali | Mkuu wa Idara ya Mipango |
| 7. Rahiya Nasser | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 8. Qs. Felchismi Tesha | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 9. Njenjela Ally | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 10. Dr. Nelson Kimolo | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 11. Kassim N. Herra | Mkuu wa Idara ya Fedha |
| 12. Margareth Temu | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 13. Juvenal A. Munishi | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 14. Donald S. Jiday | Mratibu wa TASAF |
| 15. Christopher W. Kyando | Kaimu Mkuu Kitengo cha TEHAMA |
| 16. Deogratius Michael | Kaimu Mkuu wa kitengo cha Nyuki |
| 17. Clement Kabeni | Kny; Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |

MUHT.NA.01/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao kisha kufungua kikao mnamo saa 03:35 asubuhi baada ya kutimia kwaakidi lazimu ya wajumbe.

MUHT.NA.02/2021/2022 KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO

Agenda zifuatazo zilithibitishwa kuwa agenda za kikao baada ya agenda Na.7 iliyohusu "Zoezi la uwekaji alama za utambuzi (Hereni) za klelektroniki kwa ng'ombe, punda, mbuzi na kondoo" kuondolewa.

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda za Kikao
3. Kusoma na Kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 21/10/2021
4. Yatokanayo na kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mpango cha tarehe 21/10/2021
5. Taarifa ya mapokezi ya Fedha kwa kipindi cha Mwezi Oktoba, 2021
6. Taarifa ya Mapato na Matumizi katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2021
7. Taarifa kutoka TASAF
 - Taarifa ya uhawilishaji fedha vijijini kwa walengwa wa kunusuru kaya maskini, dinisha la malipo mwezi Mei, Juni, malipo ambayo yamefanyika mwezi oktoba, 2021.
 - Taarifa ya matokeo ya zoezi la uhakiki na kuthibitisha kaya zilizopitishwa na kaya ambazo hazikupitishwa kuingia katika mpango wa kunusuru kaya maskini, kipindi cha pili cha utekelezaji wa mpango
8. Mabadiliko ya matumizi ya fedha za Serikali kuu za ujenzi wa vyumba vya madarasa ya baadhi ya shule za sekondari
9. Kufunga kikao

MUHT.NA.05/2021/2022 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2021.

Iliwasilishwa taarifa iliyoonesha Fedha zilizopokelewa katika Halmashauri ya wilaya ya Kondoa kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022. jumla ya kiasi cha shilingi 5,422,003,526.56 kilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya Halmashauri ikiwemo Miradi ya UVIKO 19.

Ambapo mradi wa UVIKO 19 kiasi cha shilingi 1,290,000,000,00 kilipokelewa na fedha hizo zilitumika kwa mchanganuo ufatao.

- Kiasi cha fedha 1,000,000,000 zilitumika kwa ajili ya miradi ya madarasa (50) katika shule za sekondari (21)
- Kiasi cha shilingi 200,000,000,00 zilitumika kwa ajili ya miradi ya madarasa (10) katika shule shikizi tatu.
- Kiasi cha shilingi 90,000,000,00 zilitumika kwa ajili ya mradi wa ujenzi nyumba ya Mtumishi.

Timu ya Menejimenti ilipokea na kuridhia taarifa ya mapokezi ya fedha hizo na kuisitiza zitumike kulingana na maelekezo yaliyotolewa.


MUHT.NA. 09/2021/2022 – KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao katika majadiliano kishakufunga kikao mnamo saa 4:58 asubuhi.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA



KATIBU



MWENYEKITI

TAREHE